**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO**

---

Unapojibu Tafadhari Taja;

**Kumbu Na.BDC/15/1/VOL . XVII /178** **11/8/2025**

## TANGAZO TANGAZO TANGAZO
## YAH: UUZAJI WA VIWANJA KATIKA KATA YA LUSAHUNGA WILAYA YA BIHARAMULO

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo anawatangazia wananchi wote na Umma kwa ujumla kuwa anauza viwanja vyenye matumizi mbalimbali. Viwanja hivyo vipo Lusahunga Barabara inayounganisha nchi za Burundi, Rwanda, na Jamhuri ya Kidemkokrasia ya Kongo katika Makutano ya Barabara ya Kuelekea Bukoba, Ngara na Kahama. Viwanja hivyo vimepimwa karibu na Eneo litapojengwa Soko la Kimkakati, Ghala kubwa la kuhifadhia vyakula la Taifa pamoja na viwanja vilivyopimwa kwa matumizi ya viwanda na taasisi za umma.

Bei za viwanja hivyo kulingana na matumizi yake ni kama ifuatavyo;-

| S/NO | MATUMIZI | BEI KWA MITA/MRABA |
|---|---|---|
| 1 | Makazi pekee | Tsh 1,000 |
| 2 | Makazi na biashara | Tsh 1,200 |
| 3 | Biashara | Tsh 3,000 |
| 4 | Hotel | Tsh 5,000 |

### UTARATIBU WA UPATIKANAJI WA VIWANJA.

1. (a) Mwombaji atalazimika kufanya maombi ya kiwanja kupitia Mfumo wa **TAUSI** Moduli ya **PLOT SALES** kwa kulipia kiasi cha Tshs. 20,000 baada ya kupata **Namba ya Malipo** (Control Number).

(b) Uchaguzi wa kiwanja/viwanja utaanza baada ya siku tano tangu tarehe ya tangazo hili kutolewa yaani tarehe 17/08/2025.

(c) Malipo ya ada ya maombi ya Kiwanja ya Tsh 20,000/= yatamwezesha muombaji/waombaji kuchagua kiwanja na kupata **Namba ya Malipo** (Control Number) ya kiwanja alichochagua.



CS CamScanner

2. Malipo ya Ada ya Maombi ya Kiwanja Tsh 20,000/= yafanyike ndani ya siku saba (7), baada ya siku hizo kuisha kiwanja kilichochaguliwa kitarejea sokoni kuchaguliwa na muhitaji mwingine na hakutakuwa na taarifa zaidi kwa muombaji wa awali.

3. Kiwanja kilichochaguliwa kitatakiwa kulipiwa fedha za ununuzi asilimia ishirini na tano (25%) ndani ya Siku thelathini (30) tangu tarehe ya kukichagua, kiasi kilichobakia kitalipwa ndani ya siku sitini (60). Kushindwa kulipia fedha zote za kiwanja husika ndani ya muda huo kitapelekea kurejeshwa kwa kiwanja hicho sokoni na fedha yote ya awali iliyolipwa na mwombaji haitarejeshwa.

4. Malipo yote yatafanyika kwa kutumia Namba ya Malipo (Control Number) ambayo muombaji ataipokea kwa njia ya mfumo wakati anafanya maombi ya kiwanja.

5. Maombi ya kiwanja, ada ya maombi, pamoja na fedha za ununuzi wa kiwanja yatafanywa na muombaji/mnunuzi kwa kupitia Mfumo wa Tausi.

6. Muombaji atatakiwa kuwa na namba ya Kitambulisho cha Uraia (**NIDA**) ili kuingia kwenye mfumo wa maombi na ulipiaji wa kiwanja (**Tausi Portal**).

7. Kwa wale ambao wapo nje ya Wilaya ya Biharamulo na wanahitaji kupata maelezo ya ziada wawasiliane na Ofisi ya Mkurugenzi moja kwa moja au kupitia Idara ya Ardhi kwa ufafanuzi zaidi.

**WANANCHI WOTE MNAKARIBISHWA.**

Innocent Mbandwa Mukandala

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**BIHARAMULO**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BIHARAMULO

**Nakala:-**

Mbao zote za Matangazo na Tovuti ya
Halmashauri ya Wilaya,
**BIHARAMULO.**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), S.L.P 70, Biharamulo, Simu:0282225003, Nukushi: 0282225216,
Barua pepe: ded@biharamulodc.go.tz. Tovuti: www.biharamulodc.go.tz.

CamScanner